

Ndogo Sheria za (Kibali cha Ujenzi) za Halmashauri ya Mji wa Tarime

Tangazo la Serikali Na. 109 (linaendelea)

TANGAZO LA SERIKALI Na. 109 la tarehe 20/3/2014

SHERIA YA FEDHA SERIKALI ZA MITAA, (MAMLAKA YA MIJI)

(SURA 288)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya Kifungu Na. 6(1) na 16(1)

SHERIA NDOGO ZA (KIBALI CHA UJENZI) ZA HALMASHAURI YA MJI WA TARIME, 2013

- | | | |
|-----------------------------------|----|--|
| Jina na tarehe ya kuanza kutumika | 1. | Sheria ndogo hizi zitaitwa sheria ndogo za Kibali cha Ujenzi za Halmashauri ya Mji wa Tarime za Mwaka, 2013 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali. |
| Matumizi | 2. | Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri. |
| Tafsiri | 3. | Katika sheria ndogo hizi:-

“ <i>Afisa Mwidhiniwa</i> ” maana yake ni Mhandisi wa Ujenzi, Msanifu Majengo au Afisa yeyote wa Halmashauri anayehusika na masuala ya Ujenzi.

“ <i>Halmashauri</i> ” maana yake ni Halmashauri ya Mji wa Tarime. |

Ndogo Sheria za (Kibali cha Ujenzi) za Halmashauri ya Mji wa Tarime

Tangazo la Serikali Na. 109 (linaendelea)

“*Jengo*” Maana yake ni nyumba iwe imekamilika kujengwa au la, iliyojengwa kwa mawe, matofali mabichi au ya kuchoma, matofali ya sementi na ambayo imezekwa kwa bati, vigae au asbesto.

“*Kibali*” Maana yake ni ruhusa au idhini itakayotolewa na Halmashauri ikiruhusu ujenzi wa jengo lolote katika maeneo maalumu.

“*Maeneo maalumu*” Maana yake ni pamoja na maeneo ya Halmashauri yaliyopimwa na maeneo mengine ambayo yatatengwa na Halmashauri kuwa maeneo maalum.

“*Mkurugenzi*” Maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Tarime ikiwa ni pamoja na Afisa yeyote atakayetekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

- Kibali cha ujenzi 4.- (1) Mtu yeyote anayetaka kujenga jengo la aina yoyote katika maeneo maalum atatakiwa kuomba na kupata kibali cha ujenzi kutoka Halmashauri,
- (2) Maombi ya kibali yataambatanishwa na Ramani ya Jengo iliyochorwa na Mtaalamu wa Michoro ya majengo, Nakala ya Hati ya kiwanja kinachokusudiwa kujengwa, ada ya kibali cha ujenzi, na maelekezo mengine yatakayotolewa na Halmashauri.
- Masharti ya kibali cha ujenzi 5.- (1) Halmashauri haitatoa kibali cha ujenzi kwa Mwombaji ambaye hajatimiza masharti yafuatayo:-
- (a) Kuwasilisha Michoro ya ramani ya jengo,
- (b) Kulipa ada ya ukaguzi wa ramani ya shs. 20,000/= kwa kila Mchoro,
Awe Mmiliki halali au mwenye madaraka kwa niaba ya
- (c) Mmiliki halali wa Kiwanja au Eneo linaloombewa kibali cha Ujenzi,
- (2) Ramani zitakazowasilishwa Halmashauri zitatakiwa kuwa na vipimo vitakavyokubaliwa na Afisa Mwidhiniwa,

Ndogo Sheria za (Kibali cha Ujenzi) za Halmashauri ya Mji wa Tarime

Tangazo la Serikali Na. 109 (linaendelea)

- (3) Halmashauri itatoa kibali cha ujenzi kwa Mwombaji ndani ya siku sitini (60) tangu tarehe ya kuwasilishwa kwa maombi.
- (4) Halmashauri itatoa kibali cha ujenzi bila Masharti au kwa masharti yafuatayo kama itaona inafaa:-
- (a) Tarehe ya kuanza na kumaliza ujenzi kwa kila kibali,
 - (b) Mwombaji kutimiza wajibu fulani kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali iliyopo,
 - (c) Kulipa ada kwa mujibu wa Sheria mbalimbali,
- Muda wa kuanza Ujenzi 6. (1) Mwombaji atatakiwa kuanza na kukamilisha Ujenzi ndani ya Miaka Mitatu (3) tangu tarehe ya kibali cha Ujenzi kutolewa,
- (2) Halmashauri inaweza kurejea kwa kuongeza Muda wa kibali cha Ujenzi kwa Mwombaji aliyeomba kuongezewa muda pale itakapoona inafaa.
- Ujenzi wa majengo ya serikali 7. Bila kuathiri masharti ya Sheria Ndogo hizi Ujenzi wa majengo ya Serikali hautahitaji kulipa ada ya kibali.
- Makosa na Adhabu 8. Mtu yeyote:-
- i Atakayejenga bila kibali cha ujenzi,
 - ii Atakayejenga bila kufuata masharti ya ujenzi kwa mujibu wa sheria ndogo hizi,
 - iii Atakayechelewa kujenga ndani ya muda wa kibali,
- Atakuwa ametenda kosa, ametenda kosa na akipatikana na hatia atalipa faini isiyozidi shilingi Laki Tatu (300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Ndogo Sheria za (Kibali cha Ujenzi) za Halmashauri ya Mji wa Tarime

Tangazo la Serikali Na. 109 (linaendelea)

Nembo ya Halmashauri ya Mji wa Tarime imebandikwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio la mkutano wa Halmashauri ulioketi tarehe 19 Mwezi 6 mwaka 2014 na ilibandikwa mbele ya:

VENANCE MWAMENGO,
Mkurugenzi wa Mji wa Tarime

DAUD WANGWE,
Mhe. Mwenyekiti Halmashauri ya Mji Tarime

NAKUBALI,

Dodoma,
22 Desemba, 2014

MIZENGO P. PINDA (MB),
Waziri Mkuu